**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# HALMASHAURI YA WILAYA YA PANGANI

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA WATAALAM (CMT) KWA KIPINDI MWEZI NOVEMBA, 2021 KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA PANGANI TAREHE 07/12/2021

## A. WATAALAM WALIOHUDHURIA:

1. Ndg. Joram A. Noa -Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)
2. Bi. M.R. Nondo - Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala - Mwenyekiti
3. Mwl. Hassan Nyange – Katibu Tawala Wilaya - Katibu
4. Bw. Najim K. Mpate - Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani - Mjumbe
5. Bw Ridhiwani R. - Kny: Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili - Mjumbe
6. Bw. Twahiru Y. Mkongo – Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Nyuki - Mjumbe
7. Bw. Daudi O. Mlahagwa – Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira - Mjumbe
8. Bw. Ramadhani Zuberi - Mkuu wa Idara ya Kilimo na Ushirika - Mjumbe
9. Bw. Aristariki F. Kimario - Kaimu Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi - Mjumbe
10. Bw. Mfaume Ally - Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi - Mjumbe
11. Bi. Asnath Mtei - Mratibu TASAF - Mjumbe
12. Bw. Kaunga J. Kaunga- Kaimu Katibu TSC - Mjumbe
13. Bi. Victoria Mfinanga - Mratibu UKIMWI - Mjumbe
14. Eng. Idd Maeda - Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi - Mjumbe
15. Adv. Msaky B.R. - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria - Mjumbe
16. Bw. Elias Msuya - Mkuu wa Idara ya M/Jamii - Mjumbe
17. Bw. Waziri Mwakibolwa- Mkuu wa Idara ya Mipango - Mjumbe
18. Bw. Gordon J. Dinda - Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara - Mjumbe
19. Dkt. Maulid Majala - Mkuu wa Idara ya Afya - Mjumbe
20. Bi. Jenipher Nyahongo- Afisa Biashara - Mjumbe

.................................
**KATIBU**

.................................
**MWENYEKITI**

**TAREHE:** 03/01/2022

21. Bi. Debora Temba - Kny: Mkuu wa Idara ya E/Sekondari - Mjumbe
22. Bw. Jumbe Mbwela - Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi - Mjumbe
23. Bw. Yamwaka Gadi - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA –Mjumbe

**C. WAANDISHI**

1. Ndg. Alexander Mugeta
2. Bi. Manka Hija

**AGENDA NA. HWP/CMT/1/12/2021: KUFUNGUA KIKAO**

Katibu alitambua uwepo wa Mwenyekiti na wataalam. Aliwakaribisha wote kwa ujumla wao na kuwafahamisha kuwa kikao ni cha kawaida kitakacho jadili taarifa za mwezi Novemba, 2021. Baada ya maelezo hayo alimkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao.

Mwenyekiti alianza kwa salamu kwa wataalam. Alimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwakutanisha tena wakiwa salama. Aliwaeleza wajumbe kuwa kikao ni cha kawaida cha kipindi cha mwezi Novemba, 2021. Alitawaka wajumbe wajadili kwa kina agenda zilizo mbele yao kwa faida ya Maendeleo ya Halmashauri ya Wilaya ya Pangani. Baada ya kusema hayo, alifungua kikao mnamo Saa **10:51 Asubuhi.**

**AGENDA NA. HWP/CMT/2/12/2021: KUTHIBITISHA AGENDA**

Katibu aliwasilisha kwa Wajumbe mapendekezo ya agenda Tano (**05**) za kikao zitakazojadiliwa katika kikao kama ifuatavyo:-

1. Kufungua Kikao.
2. Kuthibitisha Agenda za kikao cha tarehe 07/12/2021.
3. Kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha kilichopita cha tarehe 09/11/2021.
4. Kujadili Yatokanayo na kikao cha tarehe 09/11/2021.
5. Kujadili taarifa ya Fedha - Mapato na Matumizi kwa mwezi Novemba, 2021.
6. Taarifa ya mapokezi ya Fedha za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO - 19 TSh. 365,725,822.51
7. Kufunga Kikao.

…………………… **KATIBU**

…………………… **MWENYEKITI**

**TAREHE :** 03/01/2022……………

Wajumbe kwa pamoja waliridhia Agenda hizo Tano (5) zijadiliwe kwenye kikao husika.

**AGENDA NA. HWP/CMT/3/12/2021: KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE: 09/11/2021**

Katibu aliwasilisha kwa Wajumbe Muhtasari wa kikao kilichopita cha tarehe **09/11/2021**, ambapo Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kupitia muhtasari huo ukurasa kwa ukurasa na walifanya marekebisho yafuatayo:-Jina la Mjumbe (7) **Victoria Mfinga** lisomeke **Victoria Mfinanga**, (10) **Ramdhani Zuberi** lisomeke **Ramadhani Zuberi** (17) **Goldon J. Dinda** lisomeke **Gordon J. Dinda**. Baada ya marekebisho hayo Wajumbe waliridhia Muhtasari huo kwa kutiwa saini na Mwenyekiti na kuwa kumbukumbu halali ya Halmashauri ya Wilaya ya Pangani.

**AGENDA NA. HWP/CMT/4/12/2021: KUJADILI YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 09/11/2021**

- **Kuhusu suala la ujenzi wa vibanda vya wafanyabiashara vilivyojengwa kinyume na utaratibu:**

**Utekelezaji, Agizo** limetekelezwa wavamizi wote wameandikiwa Barua ya kuondoka ndani ya mwezi mmoja kwenye maeneo ya wazi waliyovamia kuanzia tarehe **19/11/2021** hadi tarehe **19/12/2021**. Kwa barua tarehe **17/11/2021 yenye** Kumb. Na. **HWP/L.10/4/VOL.II/34**. Wajumbe walikubaliana na majibu hayo.

**AGENDA NA. HWP/CMT/5/12/2021: TAARIFA YA FEDHA, MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA KUISHIA MWEZI NOVEMBA, 2021**

Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara aliwasilisha taarifa hiyo ikionyesha kwamba katika mwaka wa Fedha 2020/2021, Halmashauri ya Wilaya ya Pangani ilipitisha bajeti ya kukusanya na kupokea jumla ya TSh. **15,675,474,836.00**. Makusanyo hayo yamegawanyika kama ifuatavyo: Mapato ya Ndani TSh. **1,590,539,701,** Ruzuku Mishahara TSh. **9.218,417,403.00,** Ruzuku matumizi ya kawaida TSh. **827,280,000/** na Ruzuku ya miradi ya maendeleo na wadau wengine TSh. **4,039,237,732.00**. Taarifa hiyo pia ilionyesha kuwa katika mwaka wa Fedha wa 2021/2022, Halmashauri ya Wilaya

........................ KATIBU

........................ MWENYEKITI

TAREHE : 03/01/2022..............

ya Pangani inategemea kutumia jumla ya TSh. **15,675,474,836/-** na matumizi hayo yamegawanyika kama ifuatavyo:- Mapato ya Ndani TSh. **11,590,539,701,** Ruzuku Mishahara TSh. **9.218,417,403.00,** Ruzuku matumizi ya kawaida TSh. **827,280,000/** na Ruzuku ya miradi ya maendeleo na wadau wengine TSh. **4,039,237,732.00**. Aidha, kwa upande wa Hali Halisi hadi kuishia mwezi Novemba, 2021/22, Halmashauri imeweza kukusanya kiasi cha TSh. **5,458,565,018/=** sawa na **35%** ya makisio kwa mwaka wa Fedha 2021/2022. Katika kipindi cha mwezi Novemba, 2021, Halmashauri ilikusanya na kupokea jumla ya TSh. **1,230,257,538/=** Kati ya Mapato haya TSh. **106,185,957/-** (Mapato Halisi **95,370,582/=** na Mapato ya Afya na Elimu TSh. **10,815,315)** ni mapato yaliyotokana na vyanzo vya ndani, TSh. **40,038,142/-** ni ruzuku ya Matumizi ya kawaida (OC), TSh. **645,529,200/=** ni ruzuku ya Mishahara na TSh. **438,504,239/=** ni ruzuku ya Miradi ya Maendeleo. Makusanyo ya vyanzo vya ndani pekee ni jumla ya Sh. **464,214,225/=** sawa na asilimia **29.2%** ya bajeti ya mapato ya ndani ya Halmashauri. Mapato haya yamechangiwa na baadhi ya vyanzo vya mapato kufanya vizuri kwa zaidi ya **42%** iliyopaswa kufikiwa katika makusanyo ya kufikia mwezi Novemba, 2021. Taarifa pia ilibainisha kuwa kwa kipindi cha mwezi Novemba, 2021 mwenendo wa ukusanyaji wa mapato umekuwa na changamoto mbalimbali zikiwemo Ushirikiano mdogo kutoka kwa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) pindi wanapoingia wakandarasi wa barabara na kusababisha Halmashauri kushindwa kukusanya ushuru wa vifusi na huduma, sambamba na jitihada zinazotumika katika ufuatiliaji, Kukosa takwimu sahihi za tani zilizouzwa na zao la mkonge (mauzo mkonge) na kusababisha kushuka kwa ushuru wa zao hilo, Halmashauri kuwadai wapangaji wa mali na nyumba zinazomilikiwa na Halmashauri kiasi cha TSh. **25,524,665.00** na Uchache wa watumishi katika Kitengo cha mapato kumesababisha kupunguza nguvu za ufuatiliaji na uwajibikaji wa moja kwa moja. Sambamba na changamoto hizo, taarifa pia ilionyesha kuwa Halmashauri imepanga mikakati ya kuhakikisha inatatua changamoto zilizojitokeza ikiwa ni pamoja na kuimarisha doria katika vizuizi vya ukaguzi sambamba na kutembelea Vijiji vyote na kuhakikisha kila mchimbaji wa madini ya ujenzi anakuwa na kibali kutoka Halmashauri.

Baada ya kuwasilisha taarifa hiyo, Mweka Hazina alishauri wajumbe kuelekeza

.............................. KATIBU

.............................. MWENYEKITI

TAREHE : 03/01/2022............

nguvu kwenye mapato yatokanayo na NHIF kwani bado mwenendo wa mapato sio mzuri. Alisisitiza ni vyema wakaweka utaratibu wa pamoja ili waone kama wanakusanya au la!.

Mganga Mkuu alieleza kuwa timu iliyoundwa na Mwenyekiti imeshapita kwenye vituo vyote. Alishauri ni vyema waone kwanza taarifa iliyoandaliwa na timu hiyo ili waone hali halisi, na baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe watajua kama ukusanyaji unafanyika au la!

Mkuu wa Idara ya Fedha alisema kwa ukusanyaji upande wa ngazi ya Wilaya bado hakuna kinachofanyika.

Mwenyekiti alisema kuwa kama kunahitajika nguvu wamjulishe, kwani timu iliyoundwa imechukua muda mrefu sana. Alimuagiza Mganga Mkuu alifanyie kazi suala hilo kwa kasi zaidi.

Mjumbe mwingine alishauri ifikapo nusu mwaka vyanzo ambavyo havijafikia 50% wavijadili kwa kina ili kuona changamoto zinazovikabili vyanzo hivyo, na ufuatiliaji wakaribu ufanyike. Aidha, alishauri Idara zinazohusika zijipange ili mwisho wa siku/mwaka wawe na majibu ya pamoja.

Mkuu wa Idara ya Fedha alieleza kuwa kwa upande wa Halmashauri hakuna tatizo kubwa la ukusanyaji wa mapato. Tatizo kubwa liko kwenye makusanyo ya NHIF. Changamoto nyingine ni za vibanda vya sokoni na minada. Aliendelea kueleza kuwa mazao ya bahari yanategemea hali ya hewa. Hivyo alishauri ni muhimu kuzingatia usimamizi madhubuti wakati wa msimu.

Afisa Sheria alizungumzia upande wa vibanda vya sokoni, na kueleza kuwa changamoto sio mikataba ila bado wataalam hawajaamua kujitoa kwa dhati juu ya suala hilo. Aliwashauri wajumbe/wataalam waamue kulisimamia suala hilo kwa dhati kabisa kinyume cha hapo watakuwa wanaendelea kulea tatizo.

Afisa Mifugo na Uvuvi alizungumzia kuhusu ushuru wa Mazao ya Bahari na kushauri kuwa wakati wanaunda timu ya ukusanyaji wa mapato, wanapotoa motisha wawakumbuke watendaji walioko kwenye maeneo husika (VEO na WEO) alitolea mfano Kata ya Kipumbwi ili waweze kusaidia kwa karibu katika zoezi la ukusanyaji.

..................................... 
**MWENYEKITI**

..................................... 
**KATIBU**

**TAREHE :** 03/01/2022..........

Mkuu wa Idara ya Fedha alieleza kuwa lengo kubwa ni kukusanya mapato na Mtendaji akifanya kazi ya kukusanya mapato na akaleta matokeo chanya (ongezeko) atalipwa/atapewa motisha.

Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira alisema kuwa Hoja kubwa ni posho kwa watendaji wa Vijiji na Kata. Alishauri watengeneze hoja kule kwenye Vijiji vyao ili waweze kulipwa. Aidha, uwekwe utaratibu mzuri wa kuzishawishi Serikali za Vijiji ili iwalipe posho Watendaji wa Vijiji.

Mwenyekiti alihitimisha mjadala huo kwa kushauri kuwa malalamiko yanapotokea ni vema kwa haraka yamfike Mkurugenzi Mtendaji (W) na Mweka Hazina ili yaweze kutatuliwa. Aidha, alimshauri Mganga Mkuu aongeze nguvu miongoni mwa watumishi walio chini yake ili makusanyo ya NHIF yaonekane.

Mjumbe mwingine alizungumzia kuhusu upande wa matumizi kwenye taarifa ya Fedha. Alitaka kujua kipindi hiki cha maandalizi ya bajeti waandae bajeti ya mfumo au la!

Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara aliwashauri Wakuu wa Idara waendelee kuandaa bajeti zao kulingana na mwongozo na baadae kama timu ya wataalam watakaa ili kuona jinsi ya kusaidia zile Idara ambazo hazipati OC ili wapate. Alimalizia kwa kumshauri Afisa Mipango kushughulikia suala hilo.

Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira alishauri Idara ya Utawala itengee Idara yake mafuta na Shajala. Aidha, alishauri utaratibu uwekwe ili waweze kuendelea kuendesha Idara zao na kujenga Halmashauri kwa pamoja.

Baada ya majadiliano ya kina, wajumbe kwa pamoja walikubaliana kuwa zile Idara zenye uhitaji na ambao hawana OC waombe/wapeleke madokezo yao kwa Mkurugenzi Mtendaji (W) ili aweze kuwasaidia kupitia Mapato ya Ndani.

**AGENDA NA. HWP/CMT/6/12/2021: TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO - 19 TSH. 365,725,822.51**

Mkuu wa Idara ya Mipango aliwasilisha taarifa hiyo kwa wajumbe ikionyesha Mwezi Novemba, 2021, Halmashauri ya Wilaya ya Pangani imepokea

| | |
|---|---|
| ........................................ | ........................................ |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |

**TAREHE :** 03/01/2022..........

TSh. **365,725,822.51** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Mapambano dhidi ya COVID 19 kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

1. Ujenzi wa jengo la wagonjwa walio chini ya uangalizi wa karibu (ICU) TSh. **250,000,000.00.**
2. Ujenzi wa nyumba za watumishi (3 in one) kituo kipya cha Afya Mkalamo TSh. **90,000,000.00**
3. Uhamasishaji wa chanjo ya COVID. 19 TSh. **19,211,747.00** na
4. Ufuatiliaji na usimamizi (M&) Miradi ya COVID 19.

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kuijadili kama ifuatavyo:-

Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira alishauri na kusisitiza miradi yote inayoendelea ni vema vikajengwa vyoo vya muda kwani bila kuwepo na vyoo kutahatarisha afya za binadamu yakiwemo magonjwa ya milipuko.

Mwenyekiti aliwaagiza wataalam/walezi wa Kata waendelee kuhamasisha ujengaji wa vyoo vya muda kwenye maeneo ya miradi inayoendelea.

**AGENDA NA. HWP/CMT/6/12/2021 - KUFUNGA KIKAO**

Katibu aliwashukuru wajumbe kwa michango yao na ushauri. Aliomba wataalam kujielekeza kutekeleza maagizo yanayotolewa. Baada ya maelezo hayo alimkaribisha Mwenyekiti kufunga kikao.

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe na wataaam na kuwapongeza kwa kuweza kushirikiana na kutoa michango yao kwa faida ya wananchi wa Wilaya ya Pangani. Baada ya shukrani hizo alifunga kikao mnamo Saa **12:40 Mchana.**

**U M E T H I B I T I S H W A:**

..............................
**M.R. Nondo**
**KATIBU**

..............................
**Joram A. Noa**
**MWENYEKITI**

**TAREHE:** 03/01/2022

## YATOKANAYO NA KIKAO KAMATI YA WATAALAM (CMT) CHA TAREHE 07 DESEMBA, 2021

| NA | AGENDA NA. | AZIMIO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | **AGENDA NA. HWP/CMT/5/12/2021: TAARIFA YA FEDHA, MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA KUISHIA MWEZI NOVEMBA, 2021**<br><br>- **mapato yatokanayo na NHIF :** | **Iliazimiwa tena:** Taarifa kuhusu ukusanyaji wa mapato yatokanayo na NHIF iwasilishwe kikao kijacho ili wajumbe waone hali halisi. | MGANGA MKUU (W) | |
| | - **Kuhusu Idara ambazo hazipati mgawo wa OC** | Baada ya majadiliano ya kina, wajumbe kwa pamoja **walikubaliana** kuwa zile Idara zenye uhitaji na ambazo hazipati OC waombe/wapeleke madokezo yao kwa Mkurugenzi Mtendaji ili aweze kuwasaidia kupitia Mapato ya Ndani. | MWEKA HAZINA (W) | |
| 2. | **AGENDA NA. HWP/CMT/6/12/2021: TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO - 19 TSH. 365,725,822.51**<br><br>- **Kuhusu Miradi inayoendelea Wilayani** | **Iliagizwa kuwa:** wataalam/walezi wa Kata waendelee kuhamasisha ujengaji wa vyoo vya muda kwenye maeneo ya miradi inayoendelea | WAKUU WA IDARA /WALEZI WA KATA | Agizo limezingatiwa, Kamati za Ujenzi zimejulishwa juu ya suala la ujengaji vyoo vya muda kwenye maeneo ya miradi inayoendelea. |